



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOZA ZA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA**



**Kumb.Na GDC/F.10/127/238**

**02 Disemba, 2024**

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Geita anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa, nafasi Arobaini (40) za Ajira ya Mkataba ya wakusanya Mapato katika Halmashauri ya Wilaya Geita.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania.
- ii. Awe amehitimu Kidato cha Nne na kuendelea.
- iii. Awe na Mdhamsini mwenye mali isiyo hamishika.
- iv. Awe Mwadilifu na ambaye hajawahi kukutwa na hatia Mahakamani.
- v. Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujituma bila kusimamiwa.
- vi. Awe tayari kufanya Kazi katika Kata yoyote kwa kipindi kisichopungua Mwaka Mmoja.
- vii. Awe na Umri wa kuanzia Miaka 18 hadi 45.

**KAZI NA MAJUKUMU**

1. Kukusanya Mapato ya Halmashauri ya Wilaya Geita

## **MAMBO YA JUMLA YA KUZINGATIA.**

- i. Nakala ya Cheti cha Kidato cha Nne na kuendelea.
- ii. Waombaji waambatishe Vivuli vya Vyeti vya Elimu vilivyothibitishwa na Wakili, maelezo binafsi (CV), Nakala ya Cheti cha kuzaliwa.
- iii. Katika barua ya maombi, weka Namba yako ya simu inayopatikana muda wote.
- iv. Barua zibandikwe picha mbili (2) - Passport size.
- v. Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usaili.
- vi. Maombi yote yaambatane na barua za Wadhamini Wawili zinazoonesha Mali zisizohamishika.
- vii. Mwisho wa kupokea maombi ni **16/12/2024** saa **9:30** alasiri.
- viii. Maombi yote yaelekezwe Ofisi ya Mkurugenzi Wilaya ya Geita kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W)  
Halmashauri ya Wilaya ya Geita,  
S.L.P 139,  
**GEITA**

Limetolewa na:



Karia R. Magaro

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**HALMASHAURI YA WILAYA GEITA**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA GEITA